

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA



S. L.P 1055, ARUSHA
Simu : (027) 2503538/ 2507928
Nukushi: (027) 2505973
Barua pepe: rbcarusha@pccb.go.tz
Wavuti : www.pccb.go.tz

TAARIFA KWA UMMA

ARUSHA - APRILI 29, 2021

TAARIFA YA UTENDAJI KAZI WA TAKUKURU (M) ARUSHA KWA KIPINDI CHA MWEZI JANUARI HADI MACHI 2021

Ndg. Wanahabari,

Ninawasalimu kwa jina la **Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**. Tumewaita hapa kama ilivyo ada yetu ya kushirikiana na vyombo vya habari, kuujulisha umma juu ya shughuli mbalimbali zinazofanywa na TAKUKURU.

Leo hii tuna ufahamisha umma juu ya utendaji kazi wa ofisi ya TAKUKURU Mkoa Arusha kwa kipindi cha kuanzia Januari hadi Machi 2021. Kama ilivyo ada tunatekeleza majukumu yetu kwa mujibu wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11/2007 ambayo imeainisha majukumu yetu makuu kuwa ni **Kuchunguza na kushtaki, Kuelimisha umma juu ya rushwa, na Kuzuia rushwa** kwa Kufanya tafiti na dhibiti za mianya ya rushwa katika Mashirika ya Umma na Binafsi.

Ndg. Wanahabari,

Katika utekelezaji wa majukumu hayo ya kisheria, kwa kipindi tajwa tumefanya yafuatayo:-

1. UCHUNGUZI NA MASHITAKA:

A. TAARIFA ZILIZOPOKELEWA

Kwa kipindi tajwa jumla ya taarifa **356** zilipokelewa kutoka sekta mbalimbali. Taarifa hizi zilipelekea kufunguliwa kwa majalada **68** ya uchunguzi ambayo yanaendelea katika hatua mbalimbali za uchunguzi.

Pia ushauri yakinifu umetolewa kwa malalamiko **37** yaliyoonekana kutoangukia katika Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11/2007.

B: KESI MAHAKAMANI

Kwa kipindi tajwa, TAKUKURU (M) Arusha imefungua Mashitaka mapya Tisa (**09**) Mahakamani.

Pia Mashitaka Arobaini na Nne (**44**) yaliendelea Mahakamani yakiwa katika hatua mbalimbali za kimahakama. Aidha kwa kipindi hicho Jamhuri imeshinda mashauri Sita (**06**).

2. ELIMU KWA UMMA:

TAKUKURU (M) Arusha imeendelea kufanya jitihada za kuelimisha Umma juu ya uelewa mpana wa dhana ya Rushwa na pia kuwakumbusha wananchi wajibu wao katika mapambano dhidi ya Rushwa. Uelimishaji huo ulifanyika kwa njia mbalimbali kama ifuatavyo:-

Na	KAZI ILIYOFANYIKA	IDADI
1.	SEMINA	17
2.	MIKUTANO/MIJADALA	29
3.	KUIMARISHA KLABU	43
4.	MAONESHU	06
5.	TAARIFA KWA UMMA	04

3. UZUIAJI RUSHWA

Katika kipindi cha mwezi Januari hadi Machi, 2021 TAKUKURU Mkoa wa Arusha imefanya uchambuzi wa mfumo katika utoaji wa Vibali vya Ujenzi (Building Permits) Mkoa wa Arusha ili kubaini mianya ya rushwa iliyopo na kushauri namna sahihi ya kuiziba.

MIRADI YA MAENDELEO

TAKUKURU Mkoa wa Arusha imefika na kukagua miradi ya maendeleo inayotekelezwa kwa fedha za Serikali ili kuhakikisha kuwa miradi hiyo inatekelezwa kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa. Katika kipindi tajwa jumla ya miradi ya maendeleo kumi na mbili (12) imekaguliwa ambayo ni;

- Utekelezaji wa mfuko wa Maendeleo ya Jamii Awamu ya Tatu (TASAF III),
- Ujenzi wa ofisi za Udhhibiti Ubora wa Elimu,
- Mabweni ya shule za sekondari na madarasa yote ikiwa na jumla ya thamani ya **Shilingi Bilioni 2.1 (2,147,308,494.11/-)**.

Aidha katika kipindi tajwa, ofisi ya TAKUKURU mkoani Arusha imeokoa na kurejesha fedha jumla ya **Shilingi Bilioni 1.36** ambazo ni fedha za umma na kodi za serikali zilizokuwa, ama zimechepushwa au kufanyiwa ubadhirifu na watuhumiwa mbalimbali

kinyume na Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11 ya Mwaka 2007. Fedha zote zilizookolewa zimeshakabidhiwa kwa wahusika zikiwemo Taasisi mbalimbali za Serikali.

TAKUKURU INAYOTEMBEA:

Ndg. Wanahabari,

Katika kuhakikisha kuwa ujumbe wa mapambano dhidi ya rushwa unawafikia wananchi wote, TAKUKURU Mkoa wa Arusha ina utaratibu kwa kuwafuata wananchi katika maeneo yao kwa kampeni maalum yenye jina la '**TAKUKURU inayotembea**'. Kupitia kampeni hii, tumeweza kuwafikia wananchi katika ngazi ya kata, mitaa na vijiji kwa lengo la kusikiliza kero za vitendo vya rushwa walizonazo na kuzishughulikia. Aidha kupitia kampeni hiyo, tumeweza kuwaelimisha na kuwashauri wananchi wenye changamoto zisizokuwa za rushwa,sehemu sahihi wanapoweza kupata msaada.

4. MIKAKATI YA TAKUKURU (M) ARUSHA KWA KIPINDI CHA APRILI HADI JUNI, 2021

Ndg. Wanahabari,

Mikakati ya TAKUKURU Mkoani Arusha ni kuendelea kutekeleza majukumu kwa mujibu wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na.11/2007, kuendelea kuelimisha umma sanjari na kuuhamasisha umma kushiriki mapambanao dhidi ya rushwa, na kufanya uzuiaji rushwa kwa kufuatilia kwa karibu fedha za umma zinazoelekezwa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ili kuhakikisha kuwa fedha hizo zinatumiwa kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu na kuleta matokeo chanya katika eneo husika.

5. WITO

Ndg. Wanahabari,

Ninatoa **WITO** kwa jamii na wadau wetu wote kuendelea kushirikiana nasi hasa katika kufichua vitendo vya rushwa na kuwa tayari kutoa ushahidi mahakamani pale wanapohitajika kwani jukumu hili la kupambana na rushwa ni letu wote.

KUPAMBANA NA RUSHWA NI JUKUMU LANGU.

Imetolewa na:

**James G. Ruge
MKUU WA TAKUKURU (M)
ARUSHA**